

14. Katika Ardhi Ya Mina

Mahujaji walikuwa wamekusanyika Mina. Imam Sadiq (a.s.) na maswaha- ba wake walikuwa wameketi sehemu fulani wakila zabibu zilizokuwa zimeandaliwa mbele yao.

Muombaji alitokea na kuomba sadaka. Imam alichukua zabibu na kumpa lakini alikataa kuchukua na akaomba pesa, Imam alimwambia kuwa amsamehe kwa kuwa hakuwa na pesa za kumpa. Muombaji yule akaenda zake akiwa amekasirika.

Baada ya kwenda hatua chache alijiwa na wazo na akarudi na kuomba zile zabibu. Imam sasa akakataa kumpa zile zabibu pia.

Muda mfupi baadaye muombaji mwengine alitokea na Imam alichukua zabibu ili ampatie. Alizichukua huku akisema, “Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote na ambaye amenipa riziki yangu.” Kwa kusikia matamshi hayo Imam alimwambia asubiri na akamuongezea zabibu zingine. Maskini yule alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara ya pili.

Imam alimwambia tena asubiri huku akigeuka kwa mmoja wa marafiki zake na kumuuliza, “Una kiwango gani cha pesa?” Bwana yule alitafuta mfukoni mwake na akapata takriban dirham ishirini ambazo alimpa yule muombaji kwa amri ya Imam.

Masikini yule alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara ya tatu huku akisema “Shukrani zote zimuendee Mwenyezi Mungu, Ewe Mungu wewe ndio mpaji na hauna mshirika.” Kusikia maneno hayo Imam alivua joho lake na akampa muombaji huyo. Hapo muombaji alibadilisha shukrani zake na kuzungumza mambo ya ziada ya kumshukuru Imam mwenyewe. Kisha Imam hakumpa kitu kingine na muombaji akaondoka zake.

Marafiki na maswahaba zake ambao walikuwa mahali pale walisema: “Tulidhani kuwa kama masikini huyo angeendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kama hapo awali, Imam angeendelea kumpa vitu zaidi na zaidi. Lakini alipobadilisha matamshi yake na kumshukuru Imam mwenyewe Imam hakuendelea na usaidizi wake.

Source URL:

<https://www.al-islam.org/sw/visa-vya-wachamungu-ustadh-shahid-murtadha-mutahhari/14-katika-ardhi-ya-mina>